*Mulika, Na. 43 (1), 84-97*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Athari ya Mwachano Unaotokana na Umilisi wa Kipragmatiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda

*Mukamana Helene*[1]
Chuo Kikuu cha Rwanda
na
*Bisamaza Emilien*[2]
Chuo Kikuu cha Rwanda

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.5

**Ikisiri**

Makala haya yamechunguza athari ya mwachano unaotokana na umilisi wa kipragmatiki kwa wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda. Ingawa wanafunzi wa Rwanda wanajifunza Kiswahili kuanzia mwaka wa kwanza wa shule za upili, wanakabiliwa na changamoto za kimawasiliano ikiwa ni pamoja na umilisi wa kipragmatiki. Changamoto hiyo inatokana na mizizi ya kiutamaduni na kijamii ambayo si sawa na ustadi wa kisarufi. Changamoto hizi zinatokana na mizizi ya kijamii na kiutamaduni ya kipragmatiki ambayo si sawa na ustadi wa kisarufi. Utafiti huu, uliotumia Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles na Bryne (1992), ulijikita katika kuchunguza ujumbe wa wanafunzi kwa walimu kupitia simu na hojaji. Matokeo yanaonyesha kuwa wanafunzi wa Rwanda hukiuka kanuni za kipragmatiki za Kiswahili kutokana na athari za lugha yao ya kwanza (L1). Changamoto hiyo inasababishwa na umilisi wa pragmatiki wa L1 unaowaathiri wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili (L2). Makala yanapendekeza njia za kukabiliana na changamoto hizi ili kuboresha mawasiliano ya wanafunzi katika Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Pragmatiki ni kipengele muhimu katika mawasiliano ya lugha za binadamu. Mawasiliano yanahusisha vipengele vingine vya kijamii vinavyotawala mawasiliano husika. Mojawapo ya mambo yanayotawala mawasiliano ni suala la pragmatiki ambalo hujikita katika utamaduni wa jamii. Ustadi wa pragmatiki ni kipengele cha lugha kinachotawala mawasiliano kwa kiasi kikubwa na ambacho hujihusisha na ujuzi wa kuunganisha vitendo uneni na dhima zake katika mawasiliano kulingana na muktadha husika (Barron, 2003). Stadi za pragmatiki kwa wanafunzi wa lugha ya pili si jambo rahisi sana kwa sababu wanajikuta katika hali ya kuhamisha kanuni za lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Kanuni hizo za lugha zinaweza kuwa za kiutamaduni, kimuktadha na kitabia. Hii ina maana kwamba wanafunzi wa lugha ya pili wanalazimika kufinyanga utamaduni wa

[1] **Baruapepe:** mukamahela@gmail.com
[2] **Baruapepe:** bisamazamilien@gmail.com

jamiilugha hiyo kwa ajili ya kumudu pragmatiki ya lugha lengwa. Jambo hili linawafanya kurekebisha mawasiliano yao na wazawa au wazungumzaji wa lugha ya pili katika miktadha mbalimbali. Mawasiliano ya lugha ya pili huathiriwa na mambo kadha wa kadha. Mambo hayo ni kama vile: umri, hali ya kiuchumi, hali ya darasa, msaada wa kifamilia, motisha, kiwango cha elimu, matarajio, haiba, mtazamo wa utamaduni wa ujifunzaji lugha ya pili, uwezo wa kumudu lugha ya kwanza, viigwa au vielelezo na muktadha au mazingira (ambayo yanaweza kurahisisha au kukwamisha ujifunzaji na upataji wa lugha ya pili) (Bennett, 2004).

Cohen (2014) anabainisha vigezo kadhaa vya kiutamaduni vinavyotumika katika upimaji wa umilisi wa kipragmatiki kwa mwanafunzi wa lugha ya pili. Vigezo hivi vinalenga kubainisha kile kinachotarajiwa kwa mwanafunzi wa lugha ya pili ili kuhakikisha kuwa anamudu lugha ya pili. Katika matarajio hayo, mtu huweza kupitia vipengele maalumu vinavyohusiana na matumizi ya lugha kiutamaduni na vitendo uneni katika hali na muktadha mahususi. Uwezo wa kutumia dhana hizo katika mawasiliano ni ishara nzuri ya kuonesha kwamba wanafunzi wa lugha ya pili wanajenga umilisi wa kipragmatiki kikamilifu. Aidha, Cohen anaorodhesha mambo muhimu ya kusisitiza katika maendeleo ya ustadi wa kipragmatiki kama: uwezo wa kutoa ujumbe wa rambirambi kwa wafiwa, kushukuru, ukarimu, kuomba huduma, kuomba msamaha na kutoa mwaliko miongoni mwa masuala mengine.

## 2.0 Umilisi wa Kipragmatiki

Umilisi wa kipragmatiki ni ujuzi muhimu wa kutiliwa mkazo katika matumizi ya lugha kimawasiliano. Umilisi huu unajikita katika maana za ziada zinazohusiana na ujumbe unaotolewa na mzungumzaji kwa msikilizaji. Ukuzaji na uendelezaji wa umilisi huu, unajikita katika kufafanua vipengele mbalimbali vinavyoathiri lugha katika mawasiliano. Hilliard (2017) anabainisha mambo mbalimbali yanayotumika kama kipimo cha umilisi wa kipragmatiki kwa mzungumzaji wa lugha lengwa (L2) au ya kigeni. Mambo hayo ni: kuweza kutumia usemi tendi, kuweza kuelewa na kufasili vigezo vya maana fiche, matumizi ya dhima za staha, matumizi ya dhima za uchanganuzi kilongo na uwezo wa matumizi ya mitindo ya kiutamaduni katika mazungumzo na mawasiliano ya kila siku.

Hilliard (2017) anaongeza kwamba uwezo wa kutumia usemi tendi ni uhakika wa mtu mwenye umilisi na uhodari wa kipragmatiki. Hii ni kwa sababu usemi tendi huchukuliwa kama sehemu muhimu ya pragmatiki. Kutokana na uwezo huu wa kutumia usemi tendi, mwanafunzi au mzungumzaji wa L2, analazimika kufahamu, kutambua na kutumia viwango vya kiutamaduni-jamii kwa namna sahihi.

Kujenga uwezo wa kutumia vipengele visivyo halisi kimaana ni mojawapo wa vipimo vya uhodari wa kimazungumzo kwa lugha husika. Hivyo, pragmatiki huweka pamoja vipengele au vibainishi vya isimu ndani ya mazungumzo. Pia, katika pragmatiki viashirio na viashiriwa vinarejelewa wakati wa kuchunguza

fasili za maneno ambayo hutumiwa kulingana na matarajio ya mzungumzaji na kueleweka kwa msikilizaji. Kutokana na hayo, mwanafunzi au mzungumzaji wa L2 hulazimika kutambua mbinu za kuziba pengo la maana katika sentensi na maana kwa mujibu wa mzungumzaji na msikilizaji kwa kusudio la kukariri na kuhakikisha kilichokusudiwa katika mawasiliano (Hilliard, 2017).

Maelezo dhahiri na utumiaji wa kitamathali au kitaswira katika mawasiliano yana umuhimu wake katika mazungumzo. Hii ina maana kwamba mwanafunzi wa L2 hukabiliana na jambo la kurejelea na kuhusisha maana ya mtoa ujumbe katika sentensi na ufafanuzi wa maana ya kitaswira katika maendeleo ya umilisi wa pragmatiki katika L2. Mambo haya yote humwongoza mzungumzaji wa L2 kujua hali halisi ya kimazungumzo katika lugha lengwa.

Uhusiano wa kinasaba kati ya Kiswahili na Kinyarwanda unaweza kuwa kizuizi. Ingawa baadhi ya watalaamu wanaeleza kwamba mfanano kati ya lugha lengwa na lugha chanzi hupunguza ugumu wa kujifunza lugha lengwa (Preis, 2008), kwa upande mwingine, unaweza kuwa kizingiti. Kwa mfano, Kinyarwanda na Kiswahili hufanana na kukaribiana kimaandishi na kimaana. Msamiati unaokaribiana na kufanana kimaandishi katika Kiswahili na Kinyarwanda unaweza kuwa na maana sawa kisemantiki. Katika muktadha huu, mwanafunzi wa Kinyarwanda anayejifunza Kiswahili atatambua kwa urahisi, ingawa anaweza kupata ugumu anapokutana na maneno yanayofanana kimaandishi na kutofautiana kisemantiki. Uhusiano huu wa kimaana na kiothografia una athari kubwa katika matumizi halisi ya Kiswahili. Athari hiyo huzidi wakati mwanafunzi anapotumia lugha ya Kiswahili kulingana na kanuni za kiutamaduni pale ambapo anashindwa kutofautisha lugha yake ya kwanza ambayo ni Kinyarwanda na lugha lengwa ambayo ni Kiswahili. Hivyo, kuna umuhimu wa kuchunguza vyema matumizi ya mwachano yanayotokana na athari ya umilisi wa kipragmatiki ya lugha chanzi, L1. Kwa hiyo, tumelenga kuwasaidia wanafunzi kuepuka dosari hizo na kujenga umilisi wa kipragmatiki wa Kiswahili kama lugha inayojitegemea na inayotofautiana na Kinyarwanda.

### 2.1 Mwachano katika Matumizi ya Lugha ya Pili

Giles na Ogay (2007) ambao ni watetezi wa Nadharia ya Mwachano na Makutano (NMM), wanasema kwamba mifumo ya makutano na mwachano ni ya kipekee na kibinafsi kwa kila binadamu. Hii ina maana kwamba kuamua ukaribu na umbali wa kijamii kati ya wazungumzaji ni chaguo la kipekee na kibinafsi la kila mtu. Jambo hili linajitokeza kwa watumiaji wa lugha mbili tofauti na wamiliki wa jamiilugha mbili tofauti na ndilo linalorejelewa kama michakato ya makutano na mwachano. Kwa upande mmoja, misukumo inayosababisha makutano kwa watumiaji wa lugha mbili tofauti ni nia ya kujinasibisha na kujihusisha na jamiilugha mpya. Kukubalika katika jamiilugha mpya kunasababisha kupoteza upekee na utambulisho asilia kwa mtumiaji wa L2. Kwa upande mwingine, kuna misukumo inayosababisha kutokuwa

na haja ya kujinasibisha na jamiilugha mpya na hali hiyo hujulikana kama mifumo ya mwachano (Giles na Ogay, 2007).

Tafiti mbalimbali za miaka ya 1990 kama ile ya Lafford (1995) iliyohusu kulinganisha lugha ya mawasiliano inayotumiwa na wanafunzi wa kihispania nyumbani na ugenini; na ile ya Regan (1995) iliyolenga upataji lugha ya Kifransa kwa wanafunzi wanaosomea ugenini, zilionesha kwamba mambo mengi ya kipragmatiki yakifundishwa katika L2, yanachangia katika kuendeleza na kukuza umilisi kwa wanafunzi husika. Ingawa wanafunzi wanapewa maelekezo ya kutosha kuhusu pragmatiki ya L2, wanajikuta katika hali ya kukiuka kanuni za L2 kimatumizi (Lafford, 1995; Regan, 1995). Sababu mbalimbali zinazohusishwa na ukiukaji huu ni kama uhamishaji kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa, ukosaji wa taarifa kamili katika lugha lengwa, mazoea ya lugha chanzi kimawasiliano, ukosefu wa fursa za kuwasiliana na wazungumzaji wa lugha chanzi na wale wasio asilia, mitazamo hasi dhidi ya lugha lengwa na kutopata muda wa kutosha wa kukaa katika jamii ya lugha lengwa (Bardovi-Harlig, 1999; Barron, 2002; Blum-Kulka, 1997; Kinginger na Farrell, 2004; LoCastro, 2012).

Utafiti kuhusu mchango wa umilisi wa kipragmatiki katika matumizi ya lugha ya pili uliofanywa na Bennett (2004), ulionesha kwamba wakati mwingine, wanafunzi wanaamua kwa makusudi kutofuata kanuni za kipragmatiki za L2. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba wanafunzi wa L2 wanachagua kutumia mchakato wa makutano, mchakato wa mwachano au michakato yote miwili katika matumizi ya kanuni za kipragmatiki za lugha ya pili wanayojifunza. Matumizi ya michakato hiyo hulingana na taswira yao binafsi. Kulingana na maoni ya wanapragmatiki kama Gomez-Laich (2016), LoCastro (2012), Gomez-Laich (2016) na Bardovi (1999), mchakato wa mwachano hujitokeza mara nyingi katika mawasiliano ya wanafunzi wa L2. Kama Giles na Ogay (2007) wanavyosema, matumizi ya mchakato mwachano husababisha kujitofautisha kati ya mzungumzaji wa L2 na msikilizaji asilia wa lugha lengwa.

Tafiti mbalimbali zinathibitisha kwamba matumizi ya mwachano hujitokeza sana katika mawasiliano ya L2 hasa kwa wanafunzi wa lugha lengwa. Kwa mujibu wa Ali-Issa (2003), utambulisho huchangia sana katika matumizi ya mwachano katika mawasiliano. Wanafunzi wa L2 wanahamisha mitindo mbalimbali ya lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Kulingana na matokeo ya tafiti mbalimbali zilizoendeshwa na wanapragmatiki kama Blum-Kulka (1997), Barron (2003) na Cohen (2014), wanafunzi wa L2 wanatofautiana na wazungumzaji asilia wa lugha ya pili katika matumizi ya vitendo uneni vya kukataa, kuomba huduma na matarajio mbalimbali miongoni mwa mengine (Gomez-Laich, 2016). Wahenga wa pragmatiki kama Cohen (2014) na Gomez-Laich (2016), wanajiuliza kwa nini wanafunzi wa L2 ambao wanafahamu taratibu na kanuni mbalimbali za lugha lengwa

wanaendelea kukiuka kanuni hizo na kutumia zile za L1. Jibu la swali hili linapatikana katika utambulisho wao na athari ya L1 (Gomez-Laich, 2016).

**3.0 Nadharia ya Utafiti**

Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Makutano na Mwachano (NMM) iliyoasisiwa na Giles na Bryne (1992) wakinukuliwa na Gomez-Laich (2016). Nadharia hii ilitumiwa kwa kuegemea sana pragmatiki ya mwachano na makutano kuliko isimu pale ambapo maana katika matumizi inasisitiziwa; wakati ile ya Massamba (2007) inachunguza makutano na mwachano wa isimu za lugha za Kibantu kwa ujumla. Msingi wa nadharia hii ya NMM, unalenga vipengele vya utambulisho vinavyohusishwa na kuwekwa pamoja katika kuamua mtindo wa mawasiliano kwa minajili ya mwachano au makutano ya kijamii na matokeo ya kijamii yanayotokana na uamuzi huo. Kama ilivyoelezwa hapo juu, mwanafunzi wa L2 huamua kufuata kanuni za kipragmatiki za lugha lengwa, kukataa kuzifuatilia au kuchanganya kanuni za lugha chanzi na zile za lugha lengwa. Kwa mujibu wa NMM, uamuzi huo unaweza kuwa wa makusudi au usio wa makusudi. Mwanafunzi anaweza kuwa na nia ya kujinasibisha na jamiilugha ya L2 au kutojinasibisha wakati anapotaka kujitofautisha na jamiilugha husika. Kutokana na nadharia hii, kipimo cha mshikamano wa wanajamii kuhusu lugha na utamaduni katika kubaini nguvu za utambulisho wao hufafanuliwa na kuwekwa wazi. Kwa mujibu wa nadharia hii, ni jukumu la wanajamii wenyewe kuamua kudumisha lugha yao kwa kuitumia ili iweze kuelezea amali, mielekeo ya jamii yao na jinsi lugha yao ilivyo tofauti na lugha nyingine. Katika matumizi ya L2, kila mzungumzaji huwa na uhuru wa kuchagua kujinasibisha (makutano) ama kujitofautisha (mwachano) na jamii ya lugha ya pili.

Katika makala haya, kuna maelezo ya jinsi wanafunzi wa Kiswahili wanavyokiuka kanuni za kipragmatiki za Kiswahili kulingana na mwachano unaotokana na umilisi wa kipragmatiki wa lugha yao ya kwanza unaojitokeza katika mawasiliano yao ya kila siku. Matumizi ya kaida za salamu na mawasiliano baina yao na watu wenye nyadhifa za juu na wale ambao ni wakubwa kwao kiumri zilichunguzwa.

**4.0 Mbinu za Utafiti**

Data zilizozalisha makala haya zilipatikana kupitia muundo changamani zikihusisha mwelekeo wa kitakwimu na ule wa kimaelezo. Mugenda (2008) anaeleza kuwa muundo wa kitakwimu huwa ni jaribio la mtafiti la kusaka na kupata data kutoka kwa jamii kwa lengo la kubainisha hali ya kisasa ya jamii hiyo kwa kutumia kigezo kimoja au kingine. Hivyo basi, muundo wa kitakwimu humwezesha mtafiti kupata habari katika hali halisi ya wakati wa utafiti kutoka kwa sampuli yake. Creswell na Clark (2011) wanasema kuwa muundo wa kitakwimu hulenga kumwezesha mtafiti kufahamu na kueleza mielekeo, maoni, tabia na sifa za jamii nzima kwa kutumia data zinazotokana na sampuli iliyoteuliwa.

Kwa upande mwingine, muundo wa kimaelezo unalenga ufafanuzi katika kutafuta maarifa ya kutatua tatizo fulani au kuongeza maarifa juu ya jambo fulani. Mwelekeo huu humpa mtafiti uhuru wa kutumia vipengele vya kisanaa katika mchakato wa utafiti ili apate data halisi (Ponera, 2019). Katika makala haya, watafiti walikusanya data katika Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu, kwa ajili ya kufafanua na kuweka wazi athari ya mwachano wa umilisi wa kipragmatiki kwa wanafunzi wa Kiswahili kama L2. Aidha, utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo kwa kiwango kikubwa ingawa watafiti walihitaji takwimu mbalimbali kuhusu kiwango cha makosa ya kipragamatiki yaliyofanywa na wanafunzi kupitia athari ya mwachano katika mawasiliano. Pamoja na hayo, baada ya kukusanya, kuchunguza na kuchanganua data, watafiti walitoa maelezo na ufafanuzi mwafaka kulingana na matokeo waliyoyapata.

Katika ukusanyaji wa data za utafitii huu, ujumbe uliotumwa kwa walimu wa Kiswahili ulichunguzwa. Walimu watano walishiriki katika ukusanyaji wa data pale ambapo waliombwa na kukubali kuonesha ujumbe waliotumiwa na wanafunzi wao wakiomba huduma bila kuweka wazi utambulisho wa mtoa ujumbe. Kila mwalimu alitoa ujumbe kwa idadi sawa. Ujumbe ulichaguliwa kwa unasibu bila kumakinikia kiwango cha masomo ya mwanafunzi ama jinsi yake. Sampuli ilikusudia tu ujumbe kutoka kwenye kurasa za *WhatsApp* za wanafunzi wa Kiswahili kwa walimu wao katika Ndaki ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Rwanda kwa lengo la kuchunguza athari ya mwachano katika pragmatiki ya L1 katika matumizi ya Kiswahili kama L2. Pia, hojaji zinazolenga kuchunguza sababu zinazowasukuma wanafunzi kutumia mwachano, makutano ama mchanganyiko wa makutuno na mwachano katika mawasiliano yao ya Kiswahili zilitolewa kwa wanafunzi 10. Wanafunzi hao waliteuliwa kinasibu bila kujali mwaka wa masomo ama jinsia kwa sababu tulikuwa na uhakika kwamba kila mwanafunzi wa Kiswahili katika Ndaki ya Elimu huwa na uwezo wa kueleza sababu za chaguo lake katika maamuzi ya mambo fulani.

## 4.0 Mwachano wa Umilisi wa Kipragmatiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda

Matokeo ya utafiti huu, yanaonesha kwamba baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanakiuka kanuni za kipragmatiki za kawaida za Kiswahili kupitia mchakato wa mwachano unaojitokeza katika mawasiliano yao na walimu. Ujumbe mbalimbali kupitia mtandao wa kijamii wa *WhatsApp* ulichunguzwa na kuonesha kwamba mwachano hujitokeza katika mtindo wa salamu na uombaji wa huduma. Kwa hiyo, ujumbe mbalimbali wa wanafunzi wa Kiswahili kwa walimu wao ulichunguzwa kwa kuegemea salamu zao na uombaji wa huduma. Ilionekana kwamba mwachano unajitokeza sana katika mawasiliano hayo. Data za ujumbe zilizotoka kwa wanafunzi kuelekea kwa walimu zimewasilishwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1 Mwachano na Makutano katika Matumizi ya Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi**

| Idadi ya ujumbe | Ujumbe wenye makutano | % | Ujumbe wenye mwachano | % | Ujumbe wenye mchanganyiko | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 30 | 10 | 33.4% | 18 | 60% | 2 | 6.6% |

**Chanzo:** Utafiti wa Uwandani (2023)

Kulingana na ujumbe mfupi 30 uliochunguzwa, imeonekana kwamba asilimia 60 za ujumbe zina athari za mwachano katika matumizi. Wanafunzi asilimia 60 wanaathiriwa na uhamishaji wa mtindo wa kipragmatiki wa lugha yao asilia katika mawasiliano yao ya Kiswahili. Kwa kawaida, Wanyarwanda wanatumia mtindo wa matumizi ya hali ya wingi mrejelewaji akiwa mmoja kama ishara ya heshima. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wa Kiswahili wanaathiriwa na lugha yao asilia katika matumizi ya Kiswahili. Mojawapo ya athari hiyo ni matumizi ya viambishi vya wingi mrejelewa akiwa mmoja. Athari za mwachano zinapatika katika mifano ifuatayo:

(a) … nikakuta tayari **mmeyafunga.** Kwa hiyo, nakubali uzembe na **kuwaomba mniongeze** hata dakika hamsini za kuyaweka majadiliano hayo. **Nawashukuru** sana mwalimu."

(b) … **Kumbukeni** kunipa notisi za mwaka wa kwanza kuhusu: utangulizi wa lugha na isimu pamoja na fonetiki na fonolojia …

(c) **Hamjambo** mwalimu! Mimi ni… ninajifunza katika mwaka wa pili, yaani ni SEE nina swali kuhusu mada ya nane na ya tisa ambazo nilikuwa sijazibandika(*post*) kutokana na swali nililokuwa nalo la *eLearning* kama nilivyokuwa **nikikuonyesha** jana, kutokana na muda nimeshindwa yaani kuziposti zote na hizo mbili zikabaki tu. Ningependa kuomba msaada **kwenu** wa kunisaidia. Mungu **awalinde!**

(d) **Ahsanteni**, Mungu **akulinde** na **akuwezeshe** katika mambo yote

(e) Ningependa **kuwaomba** kufungua ile mada yenye swali la mtazamo wa fasihi.

(f) Lakini mwalimu, kuingia kwenye Moodle si rahisi kwa moja wetu ndio maana **tunawaomba** kwamba ikiwezekana **mtuongezee** muda. **Asanteni!**

(g) Salama mwalimu? Nina maswali ya **kuwauliza** ili nijue taarifa zaidi …

(h) **Hamjambo** mheshimiwa mwalimu, mimi ni… nasoma mwaka wa tatu SEE.

(i) **Ahsante** ninasubiri jibu **lenu** nzuri kwetu, mungu awajalie mema.

(j) **Asanteni** Sana Mheshimiwa

(k) **Asanteni** sana

Mifano iliyoorodheshwa hapo juu, inaonesha wazi kwamba athari ya mwachano hujitokeza katika matumizi ya Kiswahili ya wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Rwanda katika Ndaki yake ya Elimu. Athari ya mwachano inadhihirika

wazi katika uchopekaji wa viambishi vya wingi katika mawasiliano wakati mrejelewaji ni mmoja tu. Mtindo huu una mizizi katika utamaduni wa lugha ya Kinyarwanda kama ilivyosemwa awali. Hivyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba wanafunzi wanaathiriwa na umilisi wa kipragmatiki wa L1. Sababu ambazo zinaweza kusababisha wazungumzaji wa L2 kuathiriwa na mwachano katika mawasiliano yao ni nyingi. Mojawapo ya sababu hizo ni kuona kwamba hawana haja ya kujinasibisha na jamii ya L2. Kwa hiyo, wanachagua kudumisha lugha yao na utamaduni wao katika L2 ambayo ni Kiswahili. Sababu nyingine inaweza kutokana na kuathiriwa na L1 na kutumia mitindo yake katika L2 bila kukusudia. Kwa kawaida, Kiswahili kinakinzana na Kinyarwanda katika matumizi ya lugha ya staha, pale ambapo Kinyarwanda hutumia uchopekaji wa viambishi vya wingi wakati msikilizaji ni mmoja na Kiswahili huwa na msamiati maalumu wa lugha ya staha badala ya uchopekaji wa viambishi vya wingi wakati mrejelewaji ni mmoja.

Watoataarifa wanaonesha wazi kwamba wanaathiriwa na utaratibu wa kutumia viambishi vya wingi wakimrejelea mwalimu mmoja. Athari hii inaonekana wazi katika matumizi ya neno **asanteni** badala ya **asante**, **hamjambo** badala ya ***hujambo*** au **shikamoo**, **lenu** badala ya **lako**, **kwenu** badala ya **kwako** miongoni mwa mengine. Aidha, badala ya kutumia nafsi ya pili ya umoja katika matumizi ya vitenzi, wanatumia moja kwa moja nafsi ya pili ya wingi wakati mwalimu anayerejelewa ni mmoja. Kwa hiyo, matumizi ya maneno kama **mtuongezee** badala ya **utuongezee**, **mmefunga** badala ya **umefunga** na **kuwaomba** badala ya **kukuomba** yanajitokeza katika mawasiliano ya wanafunzi wa Kiswahili.

### 4.1 Sababu za Utokeaji wa Mwachano wa Umilisi wa Kipragmatiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili Rwanda

Baada ya kuona kwamba mwachano unajitokeza sana katika mawasiliano ya wanafunzi wa Kiswahili, watafiti waliwauliza wanafunzi sababu zinazowasukuma kujikuta katika hali ya kutumia mwachano katika mawasiliano yao. Swali hili lilisaidia kujua mambo fulani yanayosababisha wanafunzi kutumia umilisi wa kipragmatiki wa L1 katika L2. Jedwali Na. 2 linaonesha majibu yao.

**Jedwali Na. 2: Sababu za Kuchopeka Viambishi vya Wingi katika Mawasiliano**

| Swali | Jibu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Kwa nini unachopeka viambishi vya wingi wakati unaongea na mwalimu wako? | Uzoefu wa matumizi yake katika L1 | 5 | 50 |
| | Heshima kwa mwalimu | 10 | 100 |
| | Athari ya L1 | 4 | 40 |
| | Nafanya hivi bila makusudi | 6 | 60 |
| | Sina taarifa kuhusu jinsi ya kuonyesha heshima katika Kiswahili | 6 | 60 |
| | Sielewi vizuri sababu za kufanya hivi | 4 | 40 |

**Chanzo:** Utafiti wa Uwandani (2023)

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 2, wanafunzi walionesha sababu tofauti zinazosababisha uchopekaji wa viambishi vya wingi wakati wanaongea na mwalimu mmoja. Sababu anuwai ziliorodheshwa. Wanafunzi walionesha kwamba wanafanya hivyo kwa sababu ya heshima, kuzoea kutumia mtindo huo katika L1, kutokuwa na taarifa kamili kuhusu jinsi ya kuonesha heshima katika Kiswahili, kufanya kosa hilo bila makusudi na kutoelewa wazi sababu ya kosa hilo. Watafiti wakichunguza sababu hizo zote wanaweza kusema kwamba zina uhusiano wa moja kwa moja na athari ya lugha ya kwanza katika matumizi ya L2 pamoja na athari ya utamaduni wa L1 katika matumizi ya L2. Kulingana na matokeo, matumizi ya mtindo wa lugha ya upole na staha katika L1 hupewa kipaumbele na wanafunzi. Wanafunzi wanafanya jambo hili kwa kukusudia au bila kukusudia. Kulingana na matokeo, wanafunzi wanaonesha kwamba vipengele vya kiutamaduni, na kijamii ndivyo vinachangia katika kutumia mwachano wa kipragmatiki wa lugha yao ya kwanza. Wengine wanatumia mwachano bila kukusudia au bila kujua sababu.

Kwa kuzingatia matokeo hayo, tunaweza kusema kwamba wanafunzi wanaathiriwa na mwachano unaotokana na umilisi wa kipragmatiki wa lugha yao ya kwanza wakati wanapowasiliana na walimu wao kupitia ujumbe mfupi wa *WhatsApp* kutokana na sababu mbalimbali. Ingawa sababu hizo ni nyingi, mizizi yake iko katika kipengele cha utamaduni na athari ya L1. Kwa hiyo, wanafunzi wa Kiswahili wanatumia mwachano katika mawasiliano yao na walimu bila kujua lakini hadhira inaweza kufikiria kwamba nia yao ni kuendelea kujinasibisha na lugha yao ya kwanza na kudumisha mizizi ya utamaduni wao. Kama tulivyosema awali, mwachano unajitokeza wakati mzungumzaji wa L2 anaendelea kutumia taratibu miundo ya L1 katika mawasiliano ya L2. Jambo lingine linalojitokeza kwa wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda ni kwamba hawana uelewa wa kutosha kuhusu jinsi ya kuonesha heshima inayostahili kwa Kiswahili. Kwa hiyo,

wanatumia utaratibu wa Kinyarwanda ambao wana uhakika nao. Ikumbukwe kwamba Giles na Bryne (1992) katika ufafanuzi wao wa NMM, walionesha kwamba mzungumzaji wa L2 anaweza kujinasibisha au kujitofautisha na wazawa wa lugha hiyo kwa kukusudia au bila kukusudia. Mwachano hutumiwa kwa lengo la kudumisha utambulisho, utamaduni na taratibu mbalimbali za jamiilugha hasa lugha ya kwanza. Mwachano wa kipragmatiki pia unaweza kujitokeza katika mawasiliano ya L2 kutokana na ukosefu wa neno linalofaa katika matumizi ya lugha lengwa kiutamaduni.

## 5.0 Athari ya Mwachano katika Umilisi wa Kipragmatiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili Rwanda

Matokeo ya utafiti yalibaini kwamba athari ya mwachano wa umilisi wa kipragmatiki hujitokeza sana katika mawasiliano ya wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda. Athari hiyo mbali na mambo mengine, inasababisha makosa ya kipragmatiki katika matumizi ya Kiswahili. Utafiti ulidhihirisha kwamba wanatumia taratibu tatu za kimawasiliano wakati wanapotuma ujumbe mfupi kwa walimu kwa nia ya kuomba huduma ama msaada fulani. Utaratibu wa kwanza ni kutumia mwachano unaotokana na umilisi wa kipragmatiki wa L1 katika mawasiliano yao kwa kuchopeka viambishi vya wingi wakirejelea mtu mmoja. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba wanafunzi wengi sawa na 60% wanatumia utaratibu huu. Utaratibu wa pili ni kuchanganya mwachano na makutano katika mawasiliano. Utaratibu huu unatumiwa na wanafunzi wachache kulingana na matokeo. Matokeo yanaonesha wazi kwamba wanafunzi wanaotumia utaratibu huu ni sawa na 6.6%. Utaratibu wa tatu ni ule wa kutumia makutano katika mawasiliano. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba utaratibu huu unatumiwa na wanafunzi takribani 33.4%.

Lugha ya staha ya Kinyarwanda inatofautiana na ile ya Kiswahili. Tofauti hiyo inabainishwa katika mtindo wa lugha unaotumiwa. Katika Kiswahili kuna maneno maalumu yanayotumiwa kwa lengo la kuonesha kwamba mzungumzaji ana heshima kubwa kwa msikilizaji. Mifano ya maneno haya ni pamoja na “shikamoo” kama salamu ya mdogo kwa mkubwa, “mheshimiwa” kama neno la heshima linalotangulia mawasiliano na mtu mwenye wadhifa wa juu. Kwa upande mwingine, Wanyarwanda wanatumia mtindo mwingine wa lugha unaohakikisha kwamba wana heshima kubwa kwa msikilizaji. Mojawapo ya taratibu zinazotumiwa ni uchopekaji wa viambishi vya wingi wakati mrejelewaji ni mmoja na matumizi ya maneno ya heshima kwa kuzingatia itifaki.

Ukinzani wa matumizi ya lugha ya staha katika lugha hizi mbili ndio unaochangia sana katika matokeo ya mwachano katika mawasiliano ya wanafunzi na walimu kupitia ujumbe wa simu za mkononi kwenye *WhatsApp*. Watoataarifa walisema kwamba uzoefu wao katika L1 ndio chanzo cha kuhamisha mtindo wa Kinyarwanda katika Kiswahili. Uzoefu huo unaweza kuhusishwa na athari ya

umilisi wa kipragmatiki wa L1 katika matumizi ya L2. Kwa mujibu wa NMM, hali hii inajitokeza wakati wazungumzaji wa L2 hawataki kutoka katika mazingira ya lugha yao inayoupa utambulisho wao umuhimu mkubwa, lakini pia inaweza kutokana na ukosaji taarifa kamili kuhusu jinsi ya kutumia maneno katika muktadha wa kiutamaduni wa L2 (Giles na Bryne, 1992).

Kiswahili na Kinyarwanda pia hukinzana katika maoni ya kiutamaduni na jinsi ya kumwonesha mtu kuwa unamheshimu sana. Jamiilugha ya Kiswahili huona kwamba ni vizuri kutumia maneno maalumu ya staha yanayokubalika hasa katika matumizi ya kisarufi, wakati jamiilugha ya Kinyarwanda hutumia mtindo usio wa kawaida wa kisarufi. Mtindo huu hukiuka kanuni za kisarufi na kutumia viambishi vya wingi kwa njia ya kipekee inayotofautiana kabisa na ile ya kisarufi. Sarufi ya Kinyarwanda na ile ya Kiswahili zinahimiza kutumia viambishi kulingana na idadi ya wanaorejelewa. Ndiyo maana kunakuwa na matumizi ya viambishi vya umoja na vya wingi. Viambishi vya umoja vinatumiwa wakati wa kurejelea mtu mmoja wakati vile vya wingi vinatumiwa wakati wa kurejelea watu wengi. Utaratibu huu wa kisarufi kwa upande wa Kinyarwanda unakinzana na ule wa Kiswahili na kubadilika wakati vipengele vya kijamii na kiutamaduni vinaingia katika mfumo wa mawasiliano. Katika mfumo huo wa mawasiliano katika Kinyarwanda, mtu anayelazimika kuheshimika anaonekana na kuhesabika kama mtu zaidi ya mmoja. Kwa hiyo, wanatumia viambishi vya wingi kwa kumrejelea.

Tunaweza kusema kwamba utaratibu huu una mizizi ya kiutamaduni na kijamii kuliko lugha yenyewe ingawa tunajua kwamba lugha, jamii na utamaduni huingiliana kwa kiasi kikubwa na kukamilishana. Pamoja na hayo, tunaweza kusema kwamba mazoea ya kiutamaduni yanawasukuma wanafunzi wa Kiswahili kutumia mwachano wakati wa kuwasiliana na walimu wao. Jambo hili linaweza kufanyika kwa kukusudia au bila kukusudia kutokana na kuhitaji usalama wa lugha na kutotoka katika mazingira waliyoyazoea. Kutumia mtindo wa L1 kunapandisha kujiamini kwao katika mawasiliano kwa sababu wanaheshimu amali na desturi za jamiilugha yao. Jambo hili linatokana na mazingira yao ya ujifunzaji na kuwa hawajapata muda wa kutosha wa kukaa katika mazingira ya wazawa wa L2 (Blum-Kulka, 1997; Barron, 2002). Mambo haya yanathibitishwa na watoataarifa waliosema kwamba hawana taarifa kamili kuhusu jinsi Waswahili wanavyoonesha heshima kwa mtu anayeistahili katika mawasiliano.

Matokeo pia yalionesha kwamba kuna wanafunzi ambao wanachanganya mwachano na makutano katika mawasiliano yao na walimu. Hatuna budi kusema kwamba wanachukua pande mbili katika mawasiliano yao. Kwa upande mmoja, wanajinasibisha na jamiilugha ya Waswahili na kwa upande mwingine wanajitofautisha nao na kubaki katika mazingira yao ya kawaida ya L1. Wanafunzi hawa pia wanaathiriwa na mwachano kwa kiasi kikubwa na kutumia makutano kwa kiasi kidogo kutokana na matokeo ya utafiti. Tunaweza kusema kwamba hawa

wanajaribu kujinasibisha na jamiilugha ya Kiswahili ila vizingiti vya kiutamaduni na kijamii vinawazuia kufanikiwa na kusababisha kufanya makosa ya hapa na pale ya kimawasiliano. Makosa hayo ndiyo yanayosababisha dosari za kipragmatiki katika Kiswahili.

Kwa kuzingatia NMM, wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanaathiriwa na kigezo cha mwachano na kushindwa kutumia Kiswahili ipasavyo hasa katika matumizi ya lugha ya staha. Jambo hili linasababisha kukiuka kanuni za kipragmatiki za Kiswahili. Matumizi ya lugha yenye dosari hizi yanaweza kusababisha kupotoshwa kwa ujumbe. NMM inabainisha kwamba athari hii ya mwachano huwa na mizizi katika vipengele vya kijamii na vya kiutamaduni pale ambapo mzungumzaji wa lugha ya pili huhitaji kuwa na usalama katika mawasiliano na kudumisha utambulisho na utamaduni wake katika mawasiliano ya lugha yoyote iwayo.

## 6.0 Hitimisho

Makala haya yamefafanua jinsi wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanavyoathiriwa na mwachano na kusababisha dosari za kipragmatiki katika matumizi ya Kiswahili. Ni dhahiri kwamba athari ya mwachano huwa na mizizi katika vipengele vya kijamii na kiutamaduni. Ingawa wanafunzi hawa wanafundishwa na kuhimizwa kutumia Kiswahili fasaha darasani, wana changamoto ya kutotumia lugha fasaha katika mawasiliano yao ya kila siku. Utambulisho wao unachangia kwa kiasi kikubwa katika hali hiyo, kwani unasababisha uhamishaji wa moja kwa moja wa mitindo ya L1 kwenda L2 na vipengele vya kiutamaduni katoka L1 hadi L2. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba athari ya L1 na ile ya utamaduni wa L1 ni changamoto kubwa inayozuia wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda kutumia mitindo ya kipragmatiki ya Kiswahili inayokubalika. Utafiti umeonesha kwamba wanafunzi wanahamisha mitindo ya L1 na vipengele vya utamaduni wao katika matumizi ya lugha ya staha ya Kiswahili.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, inasisitizwa kwamba wanafunzi wanapaswa kutilia mkazo zaidi katika utambulisho wa Waswahili wakiwa na nia ya kujua tofauti yake na utambulisho wa Wanyarwanda. Kwa kufanya hivyo, wanaweza kuepuka makosa ya kuhamisha mitindo mbalimbali ya Kinyarwanda katika Kiswahili. Izingatiwe kwamba ingawa lugha hizi zina mnasaba, zinatofautiana kijamii na kiutamaduni. Kwa hiyo, kuna vipengele vya kimatumizi ambavyo vinahitaji kuchunguzwa kwa umakini kwa sababu vinatofautiana zaidi. Vipengele hivyo vyenye mizizi ya kijamii na kiutamaduni kama lugha ya staha inayozingatia salamu, kushukuru na kuomba huduma vinapaswa kutiliwa maanani. Wanafunzi wanaweza kuvilinganisha na kuvilinganua ili kuwa na uelewa kuhusu mtindo unaopaswa kutumika katika mazingira mbalimbali.

**Marejeleo**

Al-Issa, A. (2003) "Sociocultural Transfer in L2 Speech Behaviors: Evidence and Motivating Factors". *International Journal of Intercultural Relations*, Juz. 27(5): 581-601. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.1016/S0147-1767(03)00055-5. Ilisomwa tarehe 30 Agosti 2023.

Bardovi, H. K. (1999) "Exploring the Interlanguage of Interlanguage pragmatics: Research Agenda of Acquisitional Pragmatic". *A Journal of Research in Language Studies*, Juz. 49(4): 677-713. Inapatikana katika https://eric.ed.gov/?id=EJ599449. Ilisomwa tarehe 15 Juni 2023.

Barron, A. (2003) *Acquisition in Interlanguage Pragmatics. Learning How to Do Things with Words in Study Abroad Context.* Amsterdam/Philadelphia: Benjamins. Inapatikana katika https://benjamins.com/catalog/pbns.108. Ilisomwa tarehe 8 Juni 2023.

Bennett, M. J. (2004) "Becoming Interculturally Competent". Katika J. S. Wurzel (Mh.) *Toward Multiculturalism*: *A Reader in Multicultural Education*. Newton: Intercultural Resource Corporation. Inapatikana katika https://scirp.org/reference/referencespapers?referenceid=1065215. Ilisomwa tarehe 10 Septemba 2023.

Blum-Kulka, S. (1997) "Dinner Talk: Cultural Patterns of Socialization in Family". *JNABE*, Juz.Na. 21(4):100- 117. Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/15235882.1997.10162716. Ilisomwa tarehe 30 Juni 2022.

Cohen, A. (2014) "Towards Increased Classroom Assessment of Pragmatics Ability". *Iranian Journal of Language Testing*, Juz.4 (1): 5-25. Inapatikana katika https://www.ijlt.ir/article_114390_7d55cc8e8dcd8e2428d567bc5c80147b.pdf. Ilisomwa tarehe 5 Novemba 2022.

Creswell, J. W. na Clark, P. L. V. (2011) *Designing and Conducting Mixed Method Research*. California: Prentice Hall, Inc.

Giles, H. na Bryne, J. L. (1992) "An Intergroup Approach to Second Language Acquisition". *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, Juz. 3(1): 17-40. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.1080/01434632.1982.9994069. Ilisomwa tarehe 18 Oktoba 2023.

Giles, H. na Ogay, T. (2007) *Communication Accommodation Theory*: Santa Barbara: University of California.

Gomez-Laich, M. P. (2016) "Second Language Learners' Divergence from Target Language Pragmatic Norms". *Studies in Second Language Learning and Teaching*, Juz. 6 (2): 249-269. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.14746/ssllt.2016.6.2. Ilisomwa tarehe 23 Novemba 2023.

Hilliard, A. (2017) “Twelve Activities for Teaching the Pragmatics for Complaining to L2 Learners”. *English Teaching Forum*, 1-12. Inapatikana katika https://www.researchgate .net/publication/327546312. Ilisomwa tarehe 12 Oktoba 2023.

Kinginger, C. na Farrell, K. (2004) “Assessing Development of Meta-Pragmatic Awareness in Study Abroad”. *The Interdisciplinary Journal of Study Abroad*, Juz. 10(2): 19-42. Inapatikana katika DOI:10.36366/frontiers.v10i1.131. Ilisomwa tarehe 08 Septemba 2023.

Lafford, B. A. (1995) “Getting Into, Through, and Out of a Survival Situation: A comparison of Communicative Strategies used by Students Studying Spanish Abroad and at Home”. Katika B. F Freed (Mh.) *Second language acquisition in a study abroad context*. Amsterdam: John Benjamins. kur. 97-121. Inapatikana katika http://dx.doi.org/10.1111/j.1944-9720.2011.01148.x. Ilisomwa tarehe 17 Juni 2023.

LoCastro, V. (2012) *Pragmatics for Language Educators: A Sociolinguistic Perspective.* New York: Routledge.

Massamba, D. P. B. (2007) *Kiswahili Origins and Bantu Divergence-Covergence Theory*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mugenda, A. G. (2008) S*ocial Science Research*: *Theory and Principle*. Nairobi: Applied Research & Training Services.

Ponera, A. S. (2019) *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Preis, T. (2008) *Stratégies D’apprentissage Employées par les Apprenants Débutants dans L’acquisition du FLE en Milieu Institutionnel*. Maringa: Université Estadual de Maringa.

Regan, V. (1995) “The Acquisition of Sociolinguistic Native Speech Norms: Effect of a Year Abroad on Second Language Learners of French”. Katika B. F. Freed (Mh.) *Second Language Acquisition in a Study Abroad Context*. Philadelphia: John Benjamins. kur. 245-267. Inapatikana katika https://doi.org/10.1075/sibil.9.15reg. Ilisomwa tarehe 12 Juni 2023.